**MATUMIZI YA TAMATHALI ZA SEMI ZA KISWAHILI KATIKA KAMPENI ZA KISIASA: MIFANO KUTOKA UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA, 2015,** **Mr. Ahmed Yahya Sovu**


**SUMAIT UNIVERSITY JOURNAL**



**EDITORIAL BOARD**

Prof .Yunis Abdille Musa — Chief Editor
Dr. Fowzi Mohamed Barrow — Editor

**ASSISTANT EDITORS**

Dr. Mohamed Saleh Mohamed
Dr. Nassor Hamad Bakari
Mr. Mohamed Haji Ali
Mrs. Mwanatumu Ali Hassan
Mr. Burhan Hatibu Muhunzi

**EDITORIAL ADVISORY BOARD**

Prof. Amran md. Rasli — (Chairman) SUMAIT University
Prof. Hamed Rashid Hikmany — SUMAIT University
Prof. Mustafa Adam Rushash — Zanzibar University
Prof. Al said Ahmed. — The State University of Zanzibar
Prof. Mohammed Al sheikh — The State University of Zanzibar
Prof.Msafiri Mshewa — SUMAIT University
Prof. Mohamed Ali El-Kamil — International University of Africa, Sudan
Dr. Miraji Ukuti Ussi — Commission for Tourism, Zanzibar



**The Chief Editor,**
**SUMAIT University Journal of Scientific Studies,**
**P.O. Box 1933,**
**Zanzibar, Tanzania**
**Website: http://www.sumait.ac.tz**
**Annual Subscription: USD 60 (2 issues) for institutions,**

**ISSUE NO: 4- JULY 2018/1439**

**MATUMIZI YA TAMATHALI ZA SEMI ZA KISWAHILI KATIKA KAMPENI ZA KISIASA: MIFANO KUTOKA UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA, 2015, Mr. Ahmed Yahya Sovu**

# MATUMIZI YA TAMATHALI ZA SEMI ZA KISWAHILI KATIKA KAMPENI ZA KISIASA: MIFANO KUTOKA UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA, 2015

**Mr. Ahmed Yahya Sovu**

Abstract

Electoral campaigns are a means of communicating with voters where politicians enter the market for persuade their policies to voters (Wei, 2001). Politicians all over the world embellish their language in a unique way to give extra effect and force to their message in order to archive their objective of winning more votes. This article aimed at examines the use of figures of speech in political campaigns and show how they help politicians fulfill their goal of winning the elections and contribute to pushing for the community's solidarity. Data for this article has been collected in the fields and library through the analysis of documentation and interview. Data was analyzed by the approach of discourse analysis, which emphasizes that text can be analyzed through dialogue and social contexts. This article have noted that politicians have used figures of speech including, metaphor, satire, allusion, metonym, irony, simile, personification, rhetoric and euphemism in 2015 election campaigns to fulfill their goals and to show solidarity for their community. This study has contributed to sociolinguistics studies.

**Ikisiri**

Makala haya yamechunguza matumizi ya tamathali za semi za Kiswahili katika kampeni za uchaguzi mkuu wa Tanzania mwaka 2015, huku tukionesha namna ambavyo wanasiasa wamezitumia kutimiza malengo yao, ambayo ni kushinda uchaguzi. Data zimekusanywa uwandani na maktabani kwa kupitia njia ya

uchambuzi wa nyaraka na usaili. Uchambuzi wa data umeongozwa na Mkabala wa *Uchanganuzi Kilongo.* Mkabala huu unasisitiza kuwa, uchambuzi wa matini hufanywa kwa kuhusisha muktadha wa mazungumzo na hali ya kijamii. Matokeo katika makala haya yanaonesha kuwa wanasiasa wametumia tamathali za semi za *sitiari, kinaya, mdokezo, taashira, taniaba, tashbiha, tashihisi, tashititi na tasifida* katika kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015 nchini Tanzania, katika kushawishi, kuwaamsha wasikilizaji, kuwazindua, kuwavuta katika chama chao, kuwabembeleza, kuwadhoofisha wagombea wa vyama vingine ili waonekane wazembe, wavivu, wachovu, mabwege, na hatimae watimize malengo yao ya kushinda uchaguzi. makala yametoa mchango katika taaluma ya isimujamii na lugha na siasa, hususan katika kuchunguza dhima ya vipengele mbalimbali vya lugha katika kampeni za kisiasa.

## 1.0Utangulizi

Kampeni za uchaguzi ni njia ya kuwasiliana na wapiga kura ambapo wanasiasa huingia katika soko kunadi sera zao na za vyama vyao (Wei, 2001). Muktadha wa kampeni za uchaguzi ni mazingira wa wakati ambapo wanasiasa hujaribu kuwashawishi wapiga kura ili wawachague. Katika kampeni za uchaguzi wanasiasa hupamba kwa kutumia lugha ya hamasa na yenye nguvu za kimvuto ili kuwavuta wapiga kura wawachaguwe. Austin (1962) anafafanua kuwa, matamko katika nyanja ya siasa yana nguvu za aina yake. Nguvu hiyo ya lugha huwasukuma wale wenye kumsikiliza wapate mshawasha hadi kukubaliana naye. Orwell (1946) anadai kuwa, lugha ya siasa ni msuko makusudi unaotumiwa ili kuupamba uongo ili uonekane ni kweli. Aidha, lugha ni tendo-uneni linalochochewa na kufungamana na muktadha wa mazungumzo. Inawezekana kujenga mazingira yenye kuibua aina fulani ya kauli zinazokubalika katika jamii au la. Ufundi wa kuteua na kusuka lugha zinazosadifu mazingira ni moja kati ya ubunifu aliojaliwa

binadamu. Wanasiasa wazuri huwa hawatumii matusi na makonde (ngumi) kudhibiti mienendo baina ya watu, badala yake huipamba lugha na kauli zenye kuleta matokeo chanya.

Katika kutimiza malengo yao, wanasiasa huandaa mambo yafuatayo; huunda vikundi mbalimbali katika vyama vyao, vilabu na kamati, kwa lengo la kuomba kura na kufanya kampeni dhidi ya wagombea wenzao. Kampeni hizi hufanywa kupitia mikutano ya ndani na hadhara, makongamano, na mikusanyiko mingine. Miongoni mwa shughuli wanazozifanya katika kipindi hiki cha kampeni ni kuandaa hotuba, matangazo mbalimbali, kuendesha mahojiano kwa ajili ya mgombea anayewania nafasi ya kushika madaraka, kuchapisha na kusambaza majarida na vitabu mbalimbali vya ilani, mabango, vipeperushi, picha na kadhalika ambavyo vyote huwasilishwa kwa kutumia lugha yao.

Makala haya yana sehemu kuu tano. Mosi, ni utangulizi wenyewe. Pili, ufafanuzi wa dhana mbalimbali. Tatu inafafanua kuhusu mkabala wa uchambuzi wa kinadharia na nne ni kiini cha makala haya, yaani ufafanuzi wa tamathali za semi katika kampeni za uchaguzi wa mwaka 2015 na tano ni hitimisho.

## 2.0 Ufafanuzi wa Dhana Anuwai zinazohusiana na Makala

### 2.1 Dhana ya Lugha

*Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) inafasili kuwa lugha ni mfumo wa sauti za nasibu unaotumia maneno yanayosemwa na binadamu ambao huwawezesha watu wa jamii au taifa fulani kuwasiliana. Rozina (2009), anasema ili kuonesha tofauti ya dhana za *lugha* na *siasa*, kuna haja ya kuingalia fasili iliyotolewa na Chilton (2004) ambayo inaeleza kwamba, lugha ni uwezo wa kimajumui wa binadamu unaomuwezesha kuwasiliana katika jamii zote. Naye Ferdinand de Saussure (1916) ameonesha viwango vikuu vitatu vya lugha ambavyo ni, *langage*, *langue* na

*parole. Amebainisha utenda kazi katika kila kiwango na kwamba Langage* hutambulikana kama amali ya binadamu. *Langue* ni mfumo wa sheria za matumizi ya lugha mahususi. *Parole* ni utumizi binafsi wa lugha.

Kutokana na ufafanuzi huu inadhihirisha kuwa lugha ni chombo cha mwanadamu. Chombo ambacho kina vipengele vingi ndani yake yaani, vipengele vya kifonolojia, mofolojia, sintaksia na kisemantiki. Vipengele hivi hutokana na kuwa lugha hutumiwa kwa namna tofauti tofauti katika mahali tofauti, miktadha tofauti, na watu tofauti. Hata ikiwa lugha ni ile ile, tofauti inaweza kusababishwa na mambo kama vile umri, cheo, elimu na uwezo wa kiuchumi.

## 2.2 Dhana ya Siasa

Kwa upande wa siasa, *Kamusi Kuu ya Kiswahili* (2015) wanasema kuwa, siasa ni mfumo wa kiitikadi unaotumiwa na kikundi cha watu au jamii fulani kuendeshea serikali pamoja na shughuli za jamii hiyo.

Adero (2015) anaeleza kuwa siasa hujihusisha na mitafaruku na njia ya kuisuluhisha. Mitafaruku hutokana na sababu mbalimbali kama vile upungufu wa rasilimali uliosababishwa na watu wachache wenye kuhodhi rasilmali hiyo. Mtafaruku mwingine hutokana na mawazo, mitazamo, makabila, dini na utamaduni. Katika hali yoyote iwayo, lugha ndiyo chanzilishi cha mitafuruku yenyewe. Hivyo wanasiasa huitumia lugha hiyohiyo ili kuleta mshikamano pale penye utengano au kinyume yake.

## 2.3 Uhusiano Kati ya Lugha na Siasa

Ademilokun (2015) anazungumzia uhusiano wa lugha na siasa kwa kueleza kuwa, siasa ni miongoni mwa vitu halisi katika dunia yetu ya kijamii. Wakati lugha ndio muumbaji wa dunia ya kijamii. Kwamba lugha ni kama malighafi ya siasa.

**MATUMIZI YA TAMATHALI ZA SEMI ZA KISWAHILI KATIKA KAMPENI ZA KISIASA: MIFANO KUTOKA UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA, 2015,** **Mr. Ahmed Yahya Sovu**

Mtazamo kuhusu uhusiano uliopo kati ya lugha na siasa ni wa tangu enzi. Hata Ademilokun anaeleza pia kwamba, kwa mujibu wa Fairclough na Fairclough (2012:19), Aristotle ndiye aliyekuwa mtu wa mwanzo kabisa kuelezea uhusiano uliopo kati ya lugha na siasa, na mtazamo wake katika suala hili ni kwamba binadamu ni wanyama wa kisiasa na lugha ndiyo shamba ambalo wanadamu huivuna siasa hiyo. Aristotle anaeleza mtazamo huu katika nukuu kutoka kitabu chake kiitwacho *politics*

> Lakini ni jambo la kawaida kwamba binadamu ni mnyama aliyefungamana na siasa. Kama tulivyosema hapo awali, kwamba binadamu ndiye kiumbe pekee miongoni mwa wanyama ambaye ameruzukiwa kuwa na uwezo wa kuzungumza. Hivyo basi, mazungumzo ya binadamu hutawaliwa na maneno. Ni kinyume kabisa na sauti zitolewazo na wanyama wengine wakati wanapoonesha hisia zao za maumivu au furaha. Ingawa hizo sauti za wanyama hazisemwi kuwa ni lugha.
>
> Kwa upande mwingine, lugha ya binadamu husaidia kuonesha kitu chenye manufaa na chenye madhara. Lakini pia, kipi ni sahihi na kipi sio sahihi...
>
> (Tafsiri ni yetu)

Fairclough na Fairclough (watajwa) wanasisitiza kwamba mtazamo wa Aristotle wa uhusiano baina ya lugha na siasa unafafanua kwamba, Siasa ni nyenzo ya kutekeleza mambo mazuri yaliyokitwa katika kufanya uamuzi, unaotokana na makusudio yetu. Lakini, lugha ndio nyenzo kuu katika kutekeleza uamuzi wa masuala hayo nyeti ya kisiasa.

Wataalamu wengine wameendelea kueleza kuhusu uhusiano uliopo baina ya lugha na siasa. Schaffer (2004) anasisitiza kwamba, Siasa haiwezi kuendeshwa bila ya lugha. Wakati Chilton (2004) naye anashajiisha kuwa, ufanyaji wa siasa hasa umekitwa katika lugha, akimaanisha kuwa siasa itakuwa ni siasa tu kupitia lugha. Beard (2000) naye anasisitiza juu ya mtazamo huohuo kuwa, kwa kuwa lengo la siasa ni kupata mamlaka na kuyalinda mamlaka hayo basi lugha ndiyo huwa kama chombo cha kuyafikia malengo hayo. Ayeomoni (2004), akitilia nguvu muunganiko wa uhusiano baina ya lugha na siasa anaweka bayana kwamba, lugha ndiyo zana inayotumiwa katika kuieneza siasa.

Wakati mtazamo wa wataalamu hawa unaonesha kuwa mwangwi wa siasa uko katika lugha. Awonusi (2008) yeye ana mawazo kwamba, uhusiano baina ya lugha na siasa unaweza kutazamwa kwa namna tofauti na anasema kwamba, uhusiano baina ya lugha na siasa ni wa uwili-elekeani, kwa maana kwamba lugha na siasa huathiriana. Mtazamo huu unaafikiwa na Obeibi (2009), ambaye anafafanua kuwa uhusiano baina ya lugha na siasa ni wa utegemeano. Licha ya kuwa kuna mtazamo kwamba lugha ndio nyenzo kuu ya siasa, lakini matukio ya kisiasa hayaepukiki katika matukio ya kiisimu. Hivyo, ukweli unabakia kwamba siasa huathiri maumbo ya lugha, kama ilivyo lugha ya kisiasa ambayo ina vipengele vyake vinavyoifanya iwe siasa. Hata hivyo, vipengele bainishi hutegemeana katika kufikisha ujumbe uliokusudiwa.

Kwa ujumla, tunaweza kusema kwamba pamoja na mitazamo ya wataalamu hawa, ufafanuzi huu kuhusu lugha na siasa na namna vinavyohusiana, umekuwa na umuhimu sana katika kukamilisha shabaha ya makala haya. Kwa sababu, kama tulivyofafanua katika sehemu ya utangulizi, siasa inahusu upataji wa mamlaka kwa ajili ya kufanya uamuzi, kudhibiti uchumi wa nchi, na kudhibiti mienendo ya watu. Lugha, kwa mujibu wa Ayoade (1982), ndicho kiunganishi kikuu cha kufikia

mamlaka hayo, ambayo huwafikisha watu katika kuwachagua, kufanya midahalo au kufanya harakati mbalimbali. Kwa wanaisimu, kazi yao ni kuchunguza aina ya lugha, uteuzi wa maneno unaofanywa na wanasiasa katika muktadha wa kisiasa. Hasa katika kuchunguza lugha ya kisiasa imevyoweza kuonesha namna wanavyoshawishi wapiga kura hadi kushinda uchaguzi, jambo ambalo katika makala haya limelishughulikiwa.

## 2.4 Nguvu ya Lugha Kisiasa

Nguvu ya lugha ya kisiasa ni uwezo au aina ya lugha ambayo hutumiwa na wanasiasa kutimiza malengo yao ya kushika dola. Harries (1968) anadai kwamba kwa kutumia lugha unaweza kumtawala binadamu. Nae Adero (2005) anaeleza kuwa ingawa maneno yanayotumiwa na wanasiasa huwa yanaonekana ya kawaida, lakini ndani yake huwa yamejaa ushawishi. Pia, Austin (1962) anashadidia kwa kusema kuwa lugha hutumika kama chombo cha kufanya kitendo fulani kwa kutumia maneno yanayoonya, yanayouliza, yanayolazimisha, yanayoshawishi, yanayokejeli, yanayosuta, yanayoaibisha, yanayotia nguvu na yanayovunja moyo. Aidha, Beard (2000) na Charteris-Black (2005) wanatoa mfano kwamba wananchi wanapokwenda kwenye vituo vya kupigia kura kuchagua viongozi wao. Uamuzi wao wa nani wamchague au wasimchague huwa unategemea namna walivyoshawishiwa kwa kutumia lugha, kupitia hotuba za wagombea. Kwa hivyo, ndio maana tunaweza kusema kuwa lugha ina nguvu na umuhimu mkubwa katika kukamilisha malengo ya wanasiasa.

## 2.5 Mtindo wa Lugha katika Matini za Kisiasa

Mtindo wa matini za kisiasa ni jumla ya vipengele vya lugha (fonolojia, mofolojia, sintaksia na semantiki) vilivyoteuliwa na kutumiwa katika matini inayohusika (Enkvist, 1973; 1978; Haliday, 1971; Leech na Short, 1981; Traugott na Pratt, 1980). Traugott na Pratt, (1980) wanaeleza kwamba:

**MATUMIZI YA TAMATHALI ZA SEMI ZA KISWAHILI KATIKA KAMPENI ZA KISIASA: MIFANO KUTOKA UCHAGUZI MKUU WA TANZANIA, 2015,** **Mr. Ahmed Yahya Sovu**

> *"...mtindo ni matokeo ya mzungumzaji au mwandishi kuteua miundo fulani kati ya mingine mingi ambayo imo katika lugha na kuitumia katika matini inayohusika"*
>
> (Tafsiri yetu)

Kwa hivyo, mtindo wa matini za kisiasa ni jumla ya vipengele vya lugha vinavyozitambulisha matini hizo. Lasswell (1965) anaeleza kuwa mtindo katika matini za kisiasa ni namna vipengele vya lugha vinavyojidhihirisha katika mawasiliano ya kisiasa yanapofanyika, ambapo hutawaliwa na utata na mara nyingi lugha hiyo huwa haipo wazi. Kwa ufupi, lugha wanayoitumia wanasiasa huwa siyo ya bayana, lakini yenye ushawishi kwa lengo la kuendelea kumiliki rasilimali za nchi na kuendelea kushika dola (utawala). Akishadidia kuhusu mtindo wa lugha katika shughuli za kisiasa Mwansoko (1991) anaeleza kuwa lugha ya shughuli za kisiasa huwa na sifa zifuatazo; Mosi, kutoa taarifa kwa ushawishi, hii ina maana kwamba mwanasiasa hujitahidi kutoa taarifa kwa lugha ya mguso ili kuwasisimua na kuwapendeza wasikilizaji wake. Pili, hutumia msamiati mahuhusi wenye sifa za kipekee kama vile, *kuhujumu uchumi, ujamaa na kujitegemea, msaada wa hali na mali, kuzindua rasmi* . Tatu, matumizi ya tamathali za usemi, misimu, maneno ya lugha za kienyeji na za kigeni. Anaendelea kufafanua kuwa lugha inayotumiwa katika siasa huwa imepambwa vizuri ili kufanya msikilizaji awe na ari na mvuto na hujisikia kuibuliwa hisia fulani, hisia hizo zinaweza kuwa za furaha, huzuni, masikitiko, chuki na kadhalika. Mwansoko (Mtajwa) anasisitiza kwamba tamathali za usemi kama sitiari, tasfida, tashbiha, na kadhalika husaidia kuleta msisimko katika mawasiliano ya mtindo huu. Jambo ambalo limechunguzwa na makala haya, lakini kwa kuchunguza mifano kutoka katika kampeni za uchaguzi mkuu wa Tanzania mwaka wa mwaka 2015.

## 2.6 Matumizi ya Lugha katika Muktadha wa Kisiasa

Matumizi ya lugha ni namna ambavyo wazungumzaji wa lugha huitumia lugha kwa kuzingatia mila, desturi na kaida mbalimbali za jamii katika muktadha husika. Kwa kiasi kikubwa matumizi hayo ya lugha hutegemea muktadha (Masebo na Nyangwine, 2004).

Matumizi ya lugha katika muktadha wa kisiasa kama dhana, hufafanuliwa kwa namna ambavyo wanasiasa huitumia lugha kufikisha ujumbe waliokusudia kwa jamii. Kawaida, lugha ya wanasiasa hutofautiana na lugha ya kawaida (Joseph, 2006). Kwa sababu wanasiasa hutumia vipengele mbalimbali vya lugha kama vile vitendawili, hadithi, misemo,methali na pia, tamathali za semi katika kufikisha ujumbe wao kwa jamii.

## 3.0Kilongo na Uchanganuzi Kilongo

Kwa mujibu wa Candlin (1997) na Gee (2011) kilongo ni lugha katika matumizi yake, na mchakato ambao hufungamana na jamii. Fasold (1990) anafafanua kuwa, tunapochanganua kilongo huwa tunakichambua katika viwango vyote vya lugha huku tukihusisha na matumizi yake. Dhana ya kilongo huhusishwa na matini. Hii ni kwa sababu matini ni sehemu muhimu sana ya kilongo, pasi na matini huenda kilongo kisiwepo (Fairclough, 1989). Istilahi ‘kilongo’ wakati mwingine imekuwa ikirejelewa kama matini. Stubbs (1983) anaeleza kuwa kutokana na mtazamo huu huchukuliwa kuwa kilongo na matini ni dhana zinazofanana. Kwa hivyo, kilongo ni mjumuiko wa matini na muktadha wake.

Kwa ujumla kilongo kina sifa zifuatazo; Mosi, kilongo hujumuisha matini ama iwe imeandikwa au ya kuzungumza, yaani iliyohifadhiwa katika santuri ya sauti au video. Pili, kilongo hujumuisha muktadha au mazingira mahususi ambayo kuna msemaji na msemeshwaji bila kujali malengo ya mawasiliano. Katika makala haya

tumerejelea kilongo kama mchakato mzima wa mawasiliano, ambao huonyesha mpangilio wote wa mchakato wa mawasiliano na kanuni zake za maana na malengo ya muktadha wake mahususi ambao huambatana na kitu kinachosemwa au kuandikwa.

Kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa kilongo shirikishi tumewahusisha watoa matini (wagombea na viongozi wa kisiasa) na walengwa wa matini (wasikilizaji-wapiga kura) ili kubaini lengo la mzungumzaji na mapokeo ya wasikilizaji. Hali ambayo imesaidia kutimiza shabaha ya malengo ya makala haya

## 4.0 Matumizi ya Tamathali za Semi katika Kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2015

Kwa mujibu wa makala haya, tamathali za semi ni matumizi ya maneno kwa namna fulani, ili kuifanya lugha iwe ya kuvutia na kufanya jambo linalosemwa kuvutia na kupendeza kwa hadhira lengwa. Matumizi ya tamathali za semi katika kampeni za kisiasa husaidia kutia nguvu ujumbe unaofikishwa kwa wapiga kura, kwani tamathali za semi husaidia kuipamba lugha na kuongeza utamu kwa wasikilizaji. Senkoro, (2011) anasema zipo tamathali za semi nyingi sana. Ingawa katika makala haya tumechunguza baadhi tu, tena kama tulivyobaini zikitumiwa katika mikutano ya kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015.

Data za makala haya, zinatokana na usikilizaji wa hotuba za wanasiasa walizozitoa katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015, zilizoanza tangu tarehe 23/Agosti/2015 hadi 24/Agosti/2015. Data hizo tulizipakua kwa kutumia kitumizi cha "tubemate" kutoka katika mtandao wa kuhifadhia video wa "*youtube*", na kisha kuzinukuu katika maandishi. Kwa hivyo hii ni kusema kwamba, makala haya yamebainisha tamathali za semi zile tu ambazo zimebainika zinatumiwa na wanasiasa katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 bila kuzingatia vyama wanavyotoka. Katika makala haya, tunarejelea finyazo hii (KZUM)

tukimaanisha, Kampeni za Uchaguzi Mkuu. Ufuatao ni ufafanuzi wa tamathali hizo kama ifuatavyo:

### 4.1 Matumizi ya Sitiari Katika Kujilinganisha na Wapinzani wao

Kulingana na Adero (2015) sitiari huhusisha uainishaji ambapo dhana moja inahusishwa na nyingine na lugha ya ujanja hutumika. Sitiari ni sawa na tashbiha ambapo wanasiasa huzitumia kwa kulinganisha ama watu au vitu bila ya kutumia viunganishi kama vile, mithili ya, mfano wa, sawa na, na kama. Makala yamemebainisha kuwa, wanasiasa katika KZUM wa mwaka 2015 walitumia sitiari kwa lengo la kujilinganisha wao na wapinzani wao. Mfano wa 1 hapa chini unadhihirisha hilo:

(1) *...Sasa sisi tumeleta jembe, tumeleta jembe ambalo tuna uhakika kuwa kila hali tuna uhakika na tuna uwezo wa kusimama vifua mbele na kusema* ***jembe hili ni jembe chapakazi****, hili jembe limejenga zaidi ya kilomita elfu kumi na moja katika nchi hii...*

(Nape Nnauye-Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi CCM-Iringa, 28/Septemba/2015)

Katika mfano wa 1 hapo juu, tunabaini Ndugu Nape ametumia sitiari ya jembe hili ni jembe chapakazi, akijarabu kulinganisha ubora wa mgombea wa Chama cha Mapinduzi na namna jembe linavyofanya kazi ya kulima, kuchimba, kupalia na kazi nyinginezo. Kwa hivyo, ule umahiri wake na uhodari wake katika utendaji wa kazi mbalimbali za majukumu ambayo amewahi kuyashika ndizo ambazo zinafananishwa na jembe kwa kutumia kiunganishi ‘ni’.

### 4.2 Matumizi ya Kinaya katika kuwakejeli washindani wenzao

Kinaya ni tamathali ambayo wanasiasa huitumia ambapo maneno yake huwa kinyume kabisa na maana inayotakiwa kutolewa. Senkoro (2011) anasema kinaya huweza kuchanganya tamathali nyinginezo kama vile za ubeuzi uliofichika,

kinyume, tabaini na msisitizo bayani. Kinaya hutumiwa na wanasiasa kwa lengo la kuonesha dharau kwa wapinzani wao au kukemea kitendo au mtu fulani. Tazama mifano ifuatayo:

(2)*...akaambiwa kuna mchungaji mmoja anaitwa Msigwa na yeye mchungaji huyu akasema ahaa! eeh! Alisemaje? Akaambiwa alisema hivi, Niseme nisiseme? (semaaa!) Na ninamnukuu, alisema atakaye muunga mkono Lowassa aende akapimwe akili yake...(shangwe). Huu ndio ulikuwa msimamo wa Msigwa, atakayemuunga mkono Lowassa aende akapimwe nini? (akiliiiii!) Sasa Msigwa* ***tangulia mwenyewe ukapimwe akili yako mwenyewe...***

(Nape Nnauye- Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi CCM- Iringa, 28/Septemba/2015)

(3)*...CCM ikasema kwa kuwa Tanzania inahitaji kiongozi mwadilifu, ni lazima tuwapelekee kiongozi anayeakisi uadilifu kikaleta Dkt.John Pombe Magufuli...(vigelegele) wenzetu ambao walikuwa na ajenda ya kudumu ya kupiga vita ufisadi ambao walisema ni mfumo wa CCM wakaamua kuchukua* ***Wahandisi*** *na* ***Wakandarasi*** *wa ufisadi wenyewe (shangwe) wakawafanya ndio vinara...*

(Hamis Kigangwala- Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi CCM-Nzega, 17/Septemba/2015)

Katika mfano wa 2 hapo juu kuna matumizi ya maneno, tangulia mwenyewe ukapimwe akili yako mwenyewe, yametumika kuonesha kuwa alichokisema na kilichotokea ni vitu viwili tofauti.

Ama katika mfano wa 3 kuna matumizi ya maneno **Wahandisi na Wakandarasi,** ambayo katika maana ya kawaida ni watu weledi, wasomi wanaoshughulika na

masuala ya ujenzi wa barabara na majengo, lakini msemaji anawakejeli wapinzani wake kwa kusema wao ni Wahandisi na Wakandarasi wa ufisadi na sio majengo wala barabara.

Kwa jumla kinaya ni kama njia ya kumtusi mtu bila yeye kujitambua kama ametusiwa. Matumizi ya lugha ya namna hii hupunguza ukali wa maneno, na kumbe yanawakejeli wapinzani wao.

**4.3 Matumizi ya Mdokezo katika Kuleta Mshikamano**

Mdokezo ni kipengele cha kitamathali ambacho kwacho msemaji au mwandishi hukatiza maneno au huacha kitu fulani bila kukitaja au maneno ambayo kwa kawaida huwa ni wazi na huweza kujazwa kwa ubunifu (Senkoro, 2011). Katika makala haya imebainika kuwa wanasiasa katika KZUM wa mwaka 2015 walitumia mdokezo, hususani pale walipokuwa wamekerwa na jambo na wapinzani wao. Mfano wa 4 unaonesha hali hiyo:

(4) *...**Raha si raha!** (Rahaaa!) **Utamu si utamu**! (Utamuuu!) hii ndio raha CCM, wenzetu wanayo kama haya? (Hawanaa!)*

(Suleiman Sarahan Said- Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi CCM-Chanjani-Pemba,14/Oktoba/2015)

Katika mfano wa 4 hapa juu tunabaini matumizi ya mdokezo, ambapo msemaji ametumia maneno **Utamu si utamu** na **Raha si raha!** akidokeza tu bila kupambanua *utamu* au raha yenyewe iliyokusudiwa. Matumizi ya tamathali hii huleta mshawasha na hamu ya kuendelea kumsikiliza mzungumzaji kwa ule ujumbe anaoukusudia ufike kwa wapiga kura. Aidha, huleta mshikamano kwa wafuasi wake. Kwani, watu hufurahia na kila mmoja hutengeneza tafsiri ya maana ya mdokezo wake ulioachwa na msemaji wa kauli hiyo.

### 4.4 Matumizi ya Taashira katika kuaibisha Wapinzani wao

Taashira ni matumizi ya lugha ya ishara yenye lengo la kuwakilisha ujumbe fulani, ambapo jina au kitu fulani hutumika kumaanisha kitu kingine chenye uhusiano na kile kilichotumiwa. Senkoro (mtajwa) anafafanua kuwa licha ya kuwa taashira huhusu vitu, lakini ina tofauti na taniaba ambayo huhusiana na watu tu wakati taashira huhusiana na vitu. Katika makala haya imebainika kwamba, wanasiasa katika kampeni za Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015, walitumia taashira katika baadhi miktadha zilizokuwa na lengo la kuwananga (aibisha) wapinzani wao lakini kwa lugha ya uficho. Mfano wa 5 unaonesha hali hiyo:

> (5)...*hatujawahi kuuwa kwani tumeshakufa? Si tunaishi vizuri? Sumaye pamoja na vyeo vyote hutosheki? Tamaa itamuua, kutoka* ***Waziri Mkuu hadi kuwa dobi mkuu****, Lowassa hasafishiki Sumaye...*
>
> (Yusuf Makamba- Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi CCM-Morogoro, 6/Septemba/2015)

Katika mfano wa 5 hapo juu tumebaini kuwa kuna matumizi ya tamathali hii ya taashira, ambapo msemaji ametumia dhana ya dobi kwa maana ya mtu anayefua nguo na kupiga pasi nguo za watu kwa malipo ya fedha. Akimfananisha Bwana Sumaye kuwa amekuwa dobi mkuu kwa ajili ya kumsafisha Lowassa. Kauli kama hizi huwafanya wafuasi wa chama cha mgombea kuona kuwa mgombea wao ni mgombea bora, ambaye anafaa sana kuchaguliwa kuliko mgombea mwingine yeyote.

### 4.5 Matumizi ya Taniaba katika Kuonesha Tabia za Wagombea

Hii ni aina ya matumizi ya tamathali za semi ambayo kwayo jina la mtu binafsi hutumiwa kwa watu wengine wenye tabia, mwenendo wa hali au kazi sawa na ya mtu huyo. Wanasiasa katika KZUM wametumia tamathali hii ya semi hususani

katika kuonesha tabia za wagombea wao, na namna watakavyotawala mara watakapopigiwa kura. Mfano wa 6 unadhihirisha hilo:

(6)...*mjue Jakaya alikuwa anawabatiliza kwa maji, huyo ajae atawabatiliza kwa moto...*

(Yusuf Makamba-Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi CCM- Morogoro, 6/Septemba/2015 )

Katika mfano wa 6 hapo juu, imebainika kuwa mzungumzaji anamnasibisha mgombea wa CCM Ndugu John Magufuli kuwa kama Yohana mbatizaji. Katika kitabu cha Bibilia imeandikwa kwamba kulikuwa na mtu anayeitwa Yohana mbatizaji aliyebatiza kwa maji, lakini mgombea wake atabatiza kwa moto. Akimaanisha kwamba atakuwa mkali sana kuliko mtawala anayemaliza muda wake Ndugu Jakaya Kikwete. Matumizi ya tamathali hii yamesaidia kuwahamasisha wapiga kura wamuone mgombea wa CCM Ndugu Magufuli, kwamba atakaposhinda wadhifa wa urais atakuwa ni mtu jasiri na asiyetaka mchezo kama alivyokuwa Yohana Mbatizaji wa kipindi hicho cha Yesu.

### 4.6 Matumizi ya Tashbiha katika kulinganisha mambo Mbalimbali

Wanasiasa katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 wamekuwa wakitumia tashbiha kwa lengo la kulinganisha watu ama vitu viwili au zaidi kwa kutumia maneno *kama*, *mithili*, *kama kwamba* na kadhalika. Imebainika kwamba wanasiasa hutumia tashbiha kwa lengo la kujilinganisha au kuwakejeli wapinzani wao katika majukwaa ya kampeni za uchaguzi. Mfano wa 7 na wa 8 unabainisha hilo:

*(7)...Leo mtu anayesema amechoka na amani, amechoka amani ya Tanzania, amechoka umoja wetu, amechoka mshikamano wetu* ***tunamuona kama ukoma****, Kagera hoyee? ...*

(Constansia Buyeya-Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi CCM- Kagera, ITV-Habari za Saa)

(8)...*Leo mkutano wa ufunguzi* ***Wallah naona raha kama nakula tende*** *(shangwe)*...

(Borafya Ame Silima-Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi CCM-Kibandamaiti-Zanzibar, 8/Septemba/2015)

Katika mfano wa 7 hapo juu imebainika kuwa, Bi.Constansia ametumia tashibiha ya kufananisha kuwa mtu anayetaka kuvuruga hali ya amani ya nchi na mshikamano uliopo kwenye jamii, ni kama mgonjwa wa ukoma ambaye hafai hata kukaa karibu na jamii. Matumizi ya tamathali hii ya tashbiha huchagiza mshikamano kwa jamii. Kwani, suala la amani kwa maoni yetu, ni jambo la msingi sana ambapo jamii hupenda kuilinda na kuichunga kwa gharama ya aina yoyote na ikitokea kuna mtu anataka kuivurunda huchukiwa.

Katika mfano wa 8 pia, unaonesha Ndugu Borafya ametumia tashibiha katika kuonesha furaha aliyonayo katika mkutano wa ufunguzi wa chama chake, kwa hivyo ule utamu tu anaulinganisha na tunda la tende. Tunda la tende ni miongoni mwa matunda matamu sana. Kwa hivyo, anajaraibu kulingaisha raha ya kuwa katika mkutano wa chama chake na utamu wa tende.

**4.7 Matumizi ya Tashihisi katika Kuonesha Ukuu**

Kulingana na Wamitila (2008) tashihisi ni mbinu ya kutumia lugha ambapo kitu kisichokuwa na uhai kinapewa sifa za uhai. Kwa jumla, tamathali hii kwa mujibu wa Senkoro (2011) huitwa ‘Fasili ya Binadamu’ ambapo vitu visivyo na sifa walizo nazo watu hupewa sifa hizo. Wanasiasa katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 wametumia tashihisi, hasa katika kuonesha ukubwa wa vyama vyao au uwezo mkubwa alio nao mgombea wa chama chao ambapo kwa kawaida

hupambwa kwa sifa lukuki, ili kuweza kuwavutia wapiga kura. Tazama mfano wa 9 na wa 10 hapa chini:

(9)...***CCM ikasema*** *kwa kuwa Tanzania inahitaji kiongozi mwadilifu, ni lazima tuwapelekee kiongozi anayeakisi uadilifu kikaleta Dkt.John Pombe Magufuli...*

(Hamis Kingwangala- Mkutano wa Kampeni za Rais CCM – Nzega, 17/Septemba/2015)

(10)...***Ilani yetu inasema*** *tutasomesha watoto wetu kuanzia darasa la kwanza hadi kidato cha nne bila malipo, bure...*

(Samia Suluhu-Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi CCM- Iringa, 20/Oktoba/2015)

Katika mfano wa 9 hapo juu tunaona CCM, ambacho ni chama cha kisiasa, kimepewa sifa ya binadamu ya kusema hali ya kuwa uwezo wa kusema ni wa binadamu. Kwa hivyo, wanasiasa hutoa sifa hiyo ili kuonesha ukubwa wa chama na kuongeza ushirikiano na mshikamano kwa wapiga kura wao ambao huona kuwa chama chao ni chama kikubwa ambacho kinauwezo wa kutoa kauli au amri yoyote katika jamii.

Hata katika mfano wa 10 pia, inadhihirisha matumizi ya tashihisi **Ilani yetu inasema.** Kwa kweli ilani ni kitabu au waraka wenye mwongozo na mipango ya chama, kimepewa sifa ya binadamu ya kusema hali ya kuwa hakiwezi kusema.

Kwa ujumla wanasiasa hutumia tashihisi ikiwa kama njia ya kutaka kuonesha ukuu wa chama aua wagombea wao ili kuwajenga kiitikadi wafuasi wa chama chao.

### 4.8 Matumizi ya Tashititi katika kuonesha kejeli kwa wapinzani wao

Tashtiti ni mbinu ya lugha ambayo kwayo swali huulizwa hali ya kuwa jibu lake linafahamika waziwazi. Katika kampeni za uchaguzi mkuu wa mwaka 2015 wanasiasa wamekuwa wakitumia tashtiti sana katika majukwaa ya kisiasa. Utafiti huu umebaini baadhi ya tashtiti zilizotumiwa katika mikutano ya kampeni ni kama zinavyoonekana katika mfano wa 11 na wa 12 hapa chini:

> (11)...*Mimi nimekuwa Waziri Mkuu wenu kwa miaka kumi sasa, nilileta* ***maendeleo au nilileta vita?*** *Sasa nipo upande wa* ***pili mna wasiwasi tena?*** *Mheshimiwa Lowassa jemedari wetu, amekuwa Waziri na Waziri Mkuu alileta maendeleo au* ***alileta vita?*** *Kwa hiyo sasa yuko upande wa pili* ***mna wasiwasi tena?***
>
> (Fredrick Sumaye- Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi UKAWA-Sumbawanga, 29/Septemba/2015)

(12)...*Waziri Mkuu amekaa miaka miwili, kazi gani ambayo umewahi kumpa Lowassa hakutumia madaraka yake* ***vibaya na hakuiba?*** *Aniambie moja haipo, mtu mwenye historia ya namna hii chama hiki* ***kinamruhusije kwenda Ikulu?*** *Haiwezekani*...(shangwee)
(Nape Nnauye- Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi CCM-Iringa, 28/Septemba/2015)

Katika mifano ya 11 na wa 12 hapo juu, imedhihirika namna viongozi wa vyama wakitumia tashtiti, yaani wanauliza maswali katika hotuba zao lakini maswali yale hayana majibu ya moja kwa moja kutoka kwa wale wananchi wanaowaomba kura. Katika makala haya imebainika kuwa, matumizi ya tamathali ya tashtiti husaidia kuwaaminisha wapiga kura kuwa shutuma au hoja zinazotolewa kuhusu washindani wenzao kuwa ni za kweli, na huonekana kweli kwa kuwa hazijibiwi moja kwa moja katika mkutano husika. Hata hivyo wapinzani wao huwa hawapo

katika muktadha ule wa mazungumzo. Kwa kawaida tashtiti huonesha umoja na mshikamano kwani wakati mwingine jamii haipendi kujipa shida ya kutaka kujua maana na tafsiri ya kila jambo linalozungumzwa na wanasiasa, tasthiti huleta furaha moyoni mwa wapiga kura na hufurahia sana. Ingawa, wakati mwingine huwa zina kejeli ndani yake, hivyo huleta karaha.

**4.9 Matumizi ya Tasifida katika Kuficha Maudhi au Lugha kali**

Tasifida ni utumiaji wa maneno, msemo au nahau ambayo hupunguza ukali au matusi yaliyomo kwenye maneno hayo. Katika makala haya imebainishwa kuwa wanasiasa wenye busara na hekima, katika hotuba zao huwasema washindani wenzao kwa kutumia lugha ya tasifida yenye lengo la kuwahamasisha wapiga kura wamchague mgombea anayepigiwa debe, na bila kuwaudhi wapinzani wake waziwazi. Mfano wa 13 na wa 14 unadhihirisha hilo:

> *(13)...Na sote tunaijua historia ya Zanzibar na historia ya iliyokuwa Tanganyika, viongozi wetu wakubwa; wazee wetu, waanzilishi wa taifa letu; hayati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na hayati Mzee Abeid Amani Karume, wao waliungana kidete katika mapinduzi ya kuleta ukombozi wa Zanzibar na wa Tanganyika na baadaye wakaanzisha taifa jipya la Tanzania, Jamhuri ya Watu wa Zanzibar na Jamhuri ya Tanganyika na kuunda Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kwa historia hii,* ***wananchi wa Zanzibar watamuunga mkono mpaka dakika ya mwisho ya tone la mwisho la jasho yao*** *Mheshimiwa Dokta John Pombe Magufuli na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan... (makofi*)
>
> (Mohamed Shein-Mkutano wa Kampeni za Uchaguzi CCM Jangwani-DSM, 23/Agosti/2015)

> *(14)...Lakini niseme kwanza nampongeza sana, nampongeza Ndugu Magufuli kwa kazi kubwa aliyoifanya ya kuzunguka nchi nzima. Ameitembea kwa gari hakupanda helkopta.* ***Wengine wamepanda helkopta na mikutano imewashinda kuhutubia*** *(shangwe). Aliyepanda gari anapiga mkutano wa saa nzima. Anamwaga sera.* ***Anasema mwende mkasome kwenye website****. Mwananchi wa kawaida huyu, nna hakika alivyotoka mkutanoni hapa aliuliza, hivi amesema* ***twende tukasome wapi vile? Anasema website. Huko website ndio wapi?*** *Magufuli ametembea. Ameitembea nchi yote. Kwa hiyo mtakapomchagua kuwa rais, anaanza vizuri anapajua kila mahali...*

(Jakaya Kikwete- Mkutano wa Kufunga Kampeni-Jangwani, 23/Agosti/2015)

Katika mfano wa 13 hapo juu imemebainishwa kwamba msemaji ametumia tasifida. Licha ya kutumia lugha kali ya kimamlaka, badala yake ametumia lugha inayoonekana ni ya kawaida tu ambayo kaipamba na tasifida. Anasema **wananchi wa Zanzibar watamuunga mkono mpaka dakika ya mwisho ya tone la mwisho la jasho yao.** Matumizi ya lugha hii ya tafisida yamesaidia kuepusha lugha ya kuudhi kwa wapiga kura, mathalan, msemaji angeweza kusema, tutamuunga mkono ama tufe au tupone. Lakini, kwa kutumia tasifida ana epusha matumizi ya lugha pujufu.

Katika mfano 14 inaonesha matumizi ya tasifida pia, ambapo Ndugu Kikwete anatumia tasifida kumsema mgombea mwingine wa upinzani bila kumtaja, ambaye katika harakati zake za kufanya kampeni zake alitumia helkopta. Ampapo katika duru za kampeni za mwaka 2015, kuna mgombea kutokana na uchachefu wa muda hakuweza kuhutubia, kwa hivyo, akawataka wananchi waende wakasome hotuba hiyo katika 'website', yaani mtandaoni. Matumizi ya tamathali hii ya tasifida,

yamefikisha ujumbe kwa njia ya hekima ingawa kuna maneno mazito ndani yake, ambayo pia, yana aina fulani ya kijembe kwa kiongozi anayetajwa.

## 5.0 Hitimisho

Katika makala haya tumejadili kwa mifano matumizi ya tamathali za semi katika mikutano mbalimbali ya kampeni za uchaguzi wa Tanzania mwaka 2015. Tamathali za semi tulizozifafanua ni ni sitiari, kinaya, mdokezo, taashira, taniaba, tashbiha, tashihisi, tashtiti na tasifida. Kupitia tamathali hizi za semi, tumeweza kuonesha namna ambavyo kila aina ya tamthali ya semi inavyochangia katika kushawishi, kushaajiisha, kuficha, kulinganisha, kukejeli, kuonesha mshikamano, kuonesha mienendo ya watu, kupunguza ukali wa maneno na kupamba lugha kwa lengo la kuwavutia wapiga kura na hatimae kuamua ama kuwaunga mkono wagombea au la. Makala pia imejadili dhana anuwai zilizohusiana na mada kwa lengo la kujenga ufahamu wa pamoja wa masuala mbali yalizyozungumziwa katika makala haya..

Kwa kuhitimisha tunaweza kusema kuwa wanasiasa katika kampeni za kisiasa wanaweza kutumia vipengele mbalimbali vya lugha, kama vile misemeo, nahau, vitendawili, hadithi lakini pia na tamathali za semi. Ambazo kama tulivyobainisha katika makala haya zimeteuliwa na kupambwa ili zinogeshe hotuba zao hatimae waweze kuchaguliwa.

## Marejeo


- Adero, M.C (2005) "Uwezo wa Lugha katika Matini ya Siasa nchini Kenya Kuanzia 2001 hadi 2005". Tasnifu ya Umahiri (haijachapishwa), Chuo Kikuu cha Kenyata.
- Ademilokun, M. (2015) "A Multimodal Discourse Analysis of Some Newspaper Political Campaign Advertisements for Nigerian's 2015 Elections". Nigeria: Obafemi Awolowo University.
- Aduradola, R. na Ojukwu, C. (2013) "Language of Political Campaigns and Politics in Nigeria". *Canadian Social Science* 9(3):104-116.
- Aristotle, (1999) *Politics*. Kimefasiriwa na Benjamin Jowett: Batoche Books
- Ayeomoni, M.O. (2004) Linguistics-Stylistics investigation of the language of the Nigerian Political Elite. Katika Lekan Oyeleye (mh) *Language and Discourse in Society*. uk 199-213. Ibadan: Hope publication.
- Ayoade, J.A. (1982). Criteria and Constraints of conceptual and terminology analysis: An African Perspective. Katika F.W. Riggs (mh) *Proceedings of the conference on Conceptual and Terminology Analysis in the Social Sciences*. Frankfurt: Indeks Verlag.
- BAKITA, (2015) *Kamusi Kuu ya Kiswahili*. Nairobi. Longhorn
- Beard, A. (2000) *The Language of Politics*. London: Routledge.
- Brown, R na Gilman, A.L (1960) "The Pronouns of Power and Solidarity". Katika Thomas A. Sebeok (mh), Style in Language, Cambridge, MA: MIT Press, uk.253-76
- Brown, G na G. Yule, (1983) *Discourse Analysis*, Cambridge: Cambridge University Press

htpp//tubemate.net

Fairclough, I na Fairclough, N. (2012) *Political Discourse Analysis: A Method for Advance Students*. London: Routledge.

Gee, J.P (2011) *How to do Discourse Analysis: A Toolkit.* New York: Routledge.

Charteris-Black, J. (2005) *Politicians and rhetoric. The persuasive power of metaphor*. Basingstoke: Palgrave-Macmillan.

Chilton, P. na Schaffner, B. (1997) *Discourse and Politics*, London: Sage Publication.

Joseph, J. E (2006) *Language and Politics*. Edinburgh: Edinburgh University Press

Man, P. D (1984) "Epsitemology of Metaphor" Katika J. Shapiro (mh) *Language and Politics*. New York University Press: New York

Massembo, J. A na Nyangwine, N (2004) Nadharia ya Lugha ya Kiswahili 1: Kidato cha 5&6. Dar es Salaam: Afroplus Industries Ltd

Mwansoko, H. J. M. (1991) *Mitindo ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Opeib, B. (2009) *Discourse, Politics and the 1993 Presidential Election Campaigns in Nigeria: A Re-invention of June 12 Legacy*. Lagos: Nouvelle Communications Limited.

Orwell, G. (1946) "Politics and the English Language". Katika *Horizon*. Juz. 13:76.

Shapiro, M.J (1984) "Literary Production as a Politicing Practice". Katika Michael J. Shapiro (mh.) *Language and Politics*. New York University Press: New York.

Senkoro, F. (2011) *Fasihi Andishi*. Dar es Salaam. Kauttu L.t.d

Stubbs, M. (1983) *Discourse Analysis: The Socio-linguistic Analysis of Natural Language***.** Black-well Publishers.

Sylvester, J. (2016) Uchanganuzi Kilongo wa Kauli Zenye Kutweza au Kukweza Staha Katika Mijadala ya Bunge. Tasnifu ya Uzamivu (haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Tume ya Taifa ya Uchaguzi (2016) *Taarifa ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi kuhusu Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, 2015*. Dar es Salaam: Mpiga Chapa Mkuu wa serikali.

TUKI (2004) *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. (Toleo la Pili) Nairobi: Oxford University Press.

Wei, J.M.Y. (2010b) “Politeness and Politics: The Shui-Bians rhetorical Strategies: The Journal of Humanities, National Chi University 83:1-23. Katika- www.ling.sinica.edu. 2007.

Wodak, N na Meyer, M (2001) *Methods of Critical Discourse Analysis*. London: Sage

Van Dijk, T.A. (2001) *Critical Discourse Analysis*. In Tannen, D.Clifferei, D na Hamilton, H. (Wah), The Handbook of Discourse Analsis. pp 353-371.